MCHAN GO WA UTENZI WA MW ANAKUPONA KA TIKA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI MIONGONI MWA VIJANA WA LEO NCHINI UGANDA

NA

KOBUSINGYE EUDIA

2019/A/KED/0873/F

TASNIFU YA UTAFITI ILIYOWASILISHW A KATIKA KITIVO CHA ELIMU
IDARA YA LUGHA ZA KIAFRIKA KWA MALENGO YA KUTOSHELEZA BAADHI
YA MAHIT AJI YA KUKAMILISHA SHAHADA YA
SANAA KATIKA ELIMU (BAED) CHUO
KIKUU CHA KABALE

APRIL-2023

UNGAMO

Mimi, Kobusingye Eudia 2019/A/KED/0873/F ninaungama kuwa Tasinifu hii yenye mada "Mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini Uganda" ni kazi yangu asili na haijawahi kuwasilisha katika chuo kikuu kingine kwa mahitaj i ya shahada yoyote au cheti chochote.

JINA: KOBUSINGYE EUDIA

NA: 2019/A/KED/0873/F

SAHIHI __ b<>~----------

TAREHE:09/04/23

IDHINI

Tasnifu hii yenye mada, "Mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini Uganda" .imekebaliwa nami kama msimamizi aliyeteuliwa rasmi na chuo kikuu cha kabale.

JINA: **BW. AGABA INNOCENT**

SAHIHI .... ~ .. ~ ..... .

TARE HE:12/04/23

1.

TABARUKU

Kazi **hii** ninaitabarukia wazazi wangu Bwana Baryahisahe Nathan Bi Norah Baryahisahe kunisindikiza Mungu awalinde.

SHUKURANI

Ningependa kutoa shukurani zangu kwa wafuatao; kwanza nina mshukuru mwenyezi mungu kwa kunijalia uhai pamoja na kunilinda maishani hadi hiki kiwango cha elimu.Tena namshukuru msimamizi wangu Bwana Innocent Agaba kwa kweli alinitolea mwongozo katika masomo yangu pamoja na kunielekeza vile vile katika shughuli za Utafiti huu.

Wahadhiri wote chuoni cha kabale hasa wale wa Kiswahili wakiwemo Prof.Ruth Mukama,Dkt Majariwa David,Bwana Mulei Martin, ,Bw Tusimirwe Philibert,Bi Tusiime Medius,Dkt Anorld Gawasike Msigwa,na Bw Agume Innocent. Kwa kweli mlichangia sana katika kukamilisha shahada yangu ya ualimu katika chuo kikuu cha kabale, ninawatakia baraka tele za mwenyezi

mungu.

Shukurani za dhati ziwaaendelee wazazi wangu wapendwa yaani; Bw. Baryahisahe Nathani pamoja na Bi.Norah Baryahisahe ambao walinitolea malezi na pamoja kunisindikiza hadi kwa kiwango hiki cha elimu,mungu awalinde. Vile Vile,siwezi kuwasahahu Kaka zangu Bw.Mwebembezi Bruce, Kato Francis, na Byamugisha Alfred Lucky na dada zangu Bi Tushabomwe Gloriana Bi. Kesiime Caroline kwa kweli mlichangia katika kuniwezesha shahada ya ualimu katika chuo kikuu cha Kabale,Mola awazidishie kile mlichonisaidia nacho.Asante sana kabisa.

2.

YALIYOMO

UNGAMO i

IDHINI ii

TABARUKU iii

SHUKURANI iv

YALIYOMO v

SURA YA KW ANZA

UTANGULIZI

1.1 Usu Ii wa mada 1

1.2 Suala la utafiti 3

1.3 Malengo ya utafiti 3

1.3.1 Len go kuu 3

1.3.2 Malen go mahususi 3

1.4 Maswali ya utafiti: 3

1.5 Umuhimu wa utafiti 4

1.6 Upeo wa utafiti 4

1.6.1 Upeo wa wakati 4

1.6.2 Upeo wa kijiografia 4

1.7 Changamoto katika utafiti 4

SURA YA PILI MAPITIO

YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi 6

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo 6

3.

2.3 Yaliyoandikwa kuhusu uhusiano na tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa rnwanakupona na ile ya vijana wa leo 7

2.4 Yaliyoandikwa kuhusu kuchunguzajinsi uhusiano na tofauti za lugha kati ya lugha ya utenzi wa rnwanakupona zinavyoweza kuchangia kukuza na kuendeleza Kiswahili rniongoni wa vijana wa leo 9

SURA YA TATU MBINU

ZA UT AFITI

3.1 Utangulizi 11

3.2 Muundo wa utafiti **11**

3.3 Eneo la utafiti 11

3.4 Mbinu za ukusanyaaji wa data **11**

3.4.1 Ushuhudiaji 11

3.4.2 Matumizi ya maktaba 11

3.5 Sampuli na Usampulishaji **11**

3.5.1 Jurnuiya ya uteuzi wa sarnpuli **11**

3.6 Vifaa vya kukusanya data 12

3.7Utaratibu wa kukusanya data 12

3.8 Kuhakikisha ubora 12

SURA YANNE

UCHANBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

4.1 Utangulizi 13

4.2.Data kuhusu kutambua rnchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo 13

4.2. lKutumia misingi ya Kiswahili, ...13

4.2.2Uchanganyaji wa lugha, ... 14

4.2.3Mkopo wa lugha za kigeni, ... 14

4.2.4Maturnizi ya mitindo ya lugha kama vile tashibihi 14

4.

4.2.5Matumizi ya wahusika katika matumizi ya lugha 14

4.2.6Matumizi ya lugha ya kuwakilisha mazingira 14

4.3.Data kuhusu kubainisha uhusiano na tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa mwanakupona na i le ya vijana wa leo 15

4.3.1 Tofauti zilizopo kati ya mtindo wa lugha, ... , ...15

4.3.2Wahusika katika lugha, ...15

4.3.3Ugumu wa lugha, ...15

4.3.4Miaka ya lugha 16

4.3.5Idadi ya lugha za mkopo 16

4.4. Ulinganuzi wa jinsi uhusiano na tofauti za lugha katika utenzi wa mwanakupona zinavyoweza kuchangia kukuza na kuendeleza Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo 16

4.4.2Kulenga kuangaziajuu ya lugha ya Kiswahili, ... 16

4.4.2Vyote hulenga kushughulikia mtindo wa lugha, ... 17

4.4.3Kuhariri kwa lugha, ... 17

4.4.4 Miaka ya lugha ya Kiswahili 17

SURA YATANO

MUHTASARI, HITIMISHO, NA MAPENDEKEZO

5:1 Utangulizi 18

5 :2 Muhtasari 18

5.3 Hitimisho 18

5:4. Mapendekezo ya utafiti 19

5 :4.1 K wa watunga mitaala 19

5.4.2 Walimu 19

5.4.3 Kwa watafiti wa baadaya 19

MALEJELEO 19

BAJETI 21

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI

1.1 Usuli wa mada

Kijana ni mwana wa kiume au kike aliye na nguvu. Vile vile, kijana ni mtu mwenye umri kutoka miaka 13 hadi 35 kulingana na katiba ya nchi ya Uganda.

Utenzi wa Mwanakupona ulitungwa na Mwana Kupona Binti Msham, akimuusia mwanawe na kuhofu kuwa angeaga dunia kabla ya kutimiza dhima yake ya mama kama mlezi. Mama anachukua jukumu la kumpa wosia binti yake ambaye ni mchanga kiumri iii awe na uhusiano mwema na mwenyezi Mungu pamoja na mumewe. Anampa wosia kuhusu dini na hili ndilo jambo la kwanza na muhimu analomwambia. Anamwambia binti yake kwamba ashike waadhi na dini kabisa kwa sababu Mungu atamhifadhi na kumuepusha kutokana na maovu, awe na adabu aseme mambo ya kweli na ajihusishe na watu wazungumzao ukweli.

Jambo lingine ni kwamba ni bora kabisa aepukane na watu wanaozungumza mambo machafu na wajinga wasojua kujichunga. Badala yake awe marafiki na waumini na asiwapende tu wenye jamali na mali na pia asiwadharau maskini bali awasaidie. Jambo la pili ni kuhusu mumewe. Mwanakupona anamwambia binti yake amsifu mumewe siku zote watakazoishi pamoja, anaendelea kumwambia kwamba ampende mumewe kwa dhati na akitoka kwenda safari aagane naye vizuri, wakati wa kurudi amkaribishe na amtengenezee mahali pazuri pa kulala. Anaendelea kumwambia kwamba ni jukumu lake kumpikia mumewe, asimkasirikie bila sababu na asimwambie mambo mabaya.

Jambo lingine analomwambia binti yake ni kuhusu usafi. Anamwambia kwamba ni jukumu lake kufanya usafi wa kila aina kule nyumbani. Mbali na usafi wa jumla, ni vyema pia naye aoge na kuchana nywele zake vizuri kila wakati. Utenzi huu ni muhimu sana kwa sababu unawahusu vijana ambao ni wahusika wakuu Katika utafiti huu utakaohusu mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini Uganda.

1

Kiswahili kiliingia nchini Uganda mnamo mwaka wa 1844, kikafundishwa na kutumika katika mamlaka ya Kabaka Mutesa wa kwanza. Mnamo mwaka 1862, Kiswahili kilianza kuzungumzwa katika ufalme wa Bunyoro kabla ya kuja kwa wakoloni. Mnamo mwaka 1912, Kiswahili kilianza kufundishwa katika shule za msingi na upili. Mnamo mwaka 1927, Kiswahili kilipendekezwa

5.

kutumiwa na serikali ya kikoloni kama lugha rasmi na lugha ya kufundishwa shuleni (Mlacha 1995).

Mwaka 1950, serikali ya kikoloni ilipendekeza Kiswahili kuwa lugha rasmi ya kitaifa licha ya kufutilia mbali ufundishaj i wa Kiswahili shuleni mwaka 1941 kwa madai kuwa Kiswahili ni lugha ya Waarabu. Aidha, Kiswahili kilipendekezwa kufundishwa shuleni kwa ajili ya Muungano wa wafanyakazi wa Afrika Mashariki hadi mwaka 1953. Baadaye, Kamati ya De Bansen ilipinga lugha ya Kiganda au Kiswahili kuwa lugha rasmi. Haya yote yalifanyika kutokana na upinzani uliokuwepo kati ya Wamishenari na Ufalme wa Buganda kuhusiana na lugha rasmi (Mukuthuria 2006).

Baada ya Uganda kupata uhuru mnamo mwaka 1962, bunge la Uganda lilipitisha Kiswahili kufundishwa shuleni na kutumika kama lugha rasmi. Hata hivyo, uamuzi huu haukutiliwa maanani na serikali kutokana na migogoro ya kikabila (Mazrui 1995).

Mnamo mwaka 1973, Idi Amini alitangaza lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya taifa baada ya mijadala mbalimbali bungeni pamoja na upigaji wa kura ya maoni kuchagua lugha rasmi kati ya Luganda na Kiswahili. Hata baada ya Kiswahili kupitishwa kama lugha rasmi, mikakati ya utekelezaji haikuwekwa. Mnamo mwaka 1974, Kiswahili kilianza kufundishwa katika Chuo Kikuu cha Makerere. Katika mwaka 1979, serikali ya ldi Amini iliondolewa na wanajeshi wa Tanzania. Baada ya hapo, watu wakaanza kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kutangamana na wanajeshi hao. Hata hivyo, vitendo vyao vilisababisha lugha ya Kiswahili kuchukiwa na kuhusishwa na lugha ya wakatili, wezi, madikteta na kadhalika.

Licha ya kipingamizi hicho, mwaka 1986, Kiswahili kilianzishwa katika Chuo cha Ualimu Kakoba (Mlacha 1995).Mnamo mwaka 1992, Jarida la kiserikali kuhusu sera za kielimu la *Government White Paper* ilipendekeza Kiswahili kufundishwa shuleni kwa madhumuni ya Kitaifa na ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kiswahili kilipitishwa na bunge kuwa lugha rasmi mnamo mwaka 2005, mwaka 2006, 2009 na sasa ni somo la lazima katika shule za upili ngazi za nchini.

(NCDC, 2018). lngawa Kiswahili kinafundishwa kwa sasa katika vyuo kadhaa nchini Uganda, umilisi wa kiisimu kama fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki, miongoni mwa wajifunzaji, Umeripotiwa kuwa wa viwango vya chini (Jaika 2017 na Buliba 1998).

1.2 Suala la utafiti

Utenzi wa mwanakupona ni utenzi ambao umekuwa unarejelewa na wasomi au hata na jamii nzima kwa haja ya kurekebisha nidhamu za kijamii au hata na utunzi wa ndoa za kawaida, Lugha ya kiswahili chini Uganda Imeendelezwa na kukuzwa kutokana na mambo tofauti tofauti, Hivyo mtafiti ameona Kuna haja ya kutafiti juu ya mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini Uganda.

1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu pamoja na malengo mahususi kama ifuatavyo

1.3.1 Lengo kuu

Lengo kuu katika utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa VIJana wa leo nchini Uganda

1.3.2 Malengo mahususi

6. Kutambua mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo.
7. Kubainisha uhusiano na tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa mwanakupona na ile ya vijana wa leo.
8. Kuchunguza jinsi uhusiano na tofauti za lugha katika utenzi wa mwanakupona zinavyoweza kuchangia kukuza na kuendeleza kiswahili miongoni mwa vijana wa leo.

1.4 Maswali ya utafiti:

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo

i). Ni mchango gani wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona inavyoweza kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa Ieo?

ii).Ni uhusiano upi na tofauti gani zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa mwanakupona na ile ya vijana wa leo?

iii).Ni jinsi gani uhusiano na tofauti za lugha katika utenzi wa mwanakupona zinavyoweza kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo?

9.

1.5 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu unaweza kuwa na umuhimu kwa serikali, jamii, mtafiti au hata watafiti wengine kama ifuatavyo:

Utafiti huu utasaidia katika kubainisha mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa Ieo nchini Uganda.

Mbali na ukuzaji pamoja na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili, utafiti huu utasaidia katika kuwahimiza vijana katika kukuza na kutunza nidhamu baina ya familia za vijana nchini Uganda.

Utafiti huu utakuza kipawa cha mtafiti katika kufanya kazi za kiutafiti pamoja na shughuli husika nchini Uganda.

Utafiti huu utasaidia mtafiti katika kukuza ukwasi wa kutumia vifaa vya utafiti.

Kazi ya utafiti huu inaweza kutumiwa na watafiti wengine kama marejeo yao wakiwa katika wakati wa kufanya kazi za kiutafiti pamoja na shughuli hususani.

1.6 Upeo wa utafiti

Utafiti huu ulikuwa na upeo wa wakati pamoja na upeo wa kijiografia kama ifuatavyo

1.6.1 Upeo wa wakati

Utafiti huu ulitarajiwa kufanyiwa katika miezi saba.

1.6.2 Upeo wa kijiografia

Utafiti huu ulifanyiwa wilayani Rubanda Minispali ya Muko.

1.7 Changamoto katika utafiti.

Utafiti huu ulikabiliwa na changamoto zifuatazo

Vifaa vya utafiti viii kuwa ghali sana ambapo hiki kiliathiri hoja au data zilizokukusanywa.

Wakati unaotarajiwa katika kukamilisha utafiti huu unaweza kuwa finyu huku wakati pana ukihitajika katika kukamilisha utafiti.

Utafiti huu uliathiriwana wingi wa data zilizositahili kukamilisha utafiti huu, lakini utafiti huu ulijikita kwa tenzi pamoja na makala yenye uhusiano na mada iii kukamilisha utafiti huu ulikaohusu mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini Uganda

10.

Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo wazungumzaji wake huwa ni nadra sana katika maeneo ya utafiti huu, hivyo kama wanavyolengwa kama miongoni mwa wahojiwa wa utafiti huu, mtafiti alijikita kwa njia ya kutafsili kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili.

Ukosefu wa fedha ni miongoni mwa changamoto zilizoweza kukabili harakati za utafiti huu, mtafiti atakosa pesa zinazohitajika iii kukamilisha shughuli za utafiti huu

1.8. Ufafanuzi wa isitilahi muhimu

Mchango;	Msaada mwema/mvuto
Mwanakupona;	Utenzi uliotungwa zamani
Vijana;	Watu wenye umri isiyozidi miaka thelathini (30) Kazi au
Utenzi;	Makala yaliotungwajuu ya mambo tofauti.s

11.

SURA YA PILI
MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Katika sura ya pili, utafiti huu ulirejelea yaliyoandikwa na watafiti wa awali huku yakiwa na uhusiano na mada pamoja na malengo ya utafiti huu uliohusu mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini Uganda

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo

Kulingana na Kaaru, M.G. (2008) katika uchunguzi alioufanya kuhusu dhima ya ushairi katika jamii, utanzu wa ushairi ni maarufu sana katika fasihi za jamii nyingi ulimwenguni na umeendelea kuwapo kwa kuwa jamii inanufaishwa mno nao. Kwa mfano, katika jamii ya Waswahili ushairi ni maarufu sana na wenyewe una historia ndefu mno. Awali mashairi yalitongolewa majukwaani, kazini na faraghani kama fani ya fasihi simulizi. Hata hivyo, katika utekelezaji wake aliendelea kueleza kuwa Ushairi hutekeleza majukumu mbali mbali katika jamii. Miongoni mwa majukumu aliyotaja ni kwamba huhifadhi matukio muhimu ya historia ya jamii. Mashairi ni kumbukumbu za mambo yaliyowahi kumpata mwanadamu katika awamu mbalimbali za maisha. Kwa mfano biashara, utumwa, ukoloni, dini mpya, vita, uhuru na matendo ya mashujaa na watu wengine mashuhuri. Kwa mfano, utenzi wa AI-Inkishafi unaeleza historia ya mji wa Pate tangu mwanzo, kustawi kwake, hadi kuporomoka.

Maoni yake Kaaru (2008) yatakuwa muhimu katika utafiti huu wetu, kwani yanaeleza dhima ya ushairi katika jamii kwa kusema kuwa utanzu wa ushairi ni maarufu sana katika fasihi za jamii nyingine ulimwenguni. Kutofautiana kunajitokeza pale ambapo amejumuisha shairi bila kutaja vipengele vya ndani vya lugha vinaposhughulikiwa katika shairi, lakini katika uchunguzi wake alijikita kwa utenzi wa Al- Inkishafi kwa kutoa mfano, hiki kitaendelea kurejelewa sana katika utafiti huu iii kutambua mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo.

Chimerah (2011), katika uchunguzi alioufanya kuhusu nyimbo kama kifaa cha kujifunza Kiswahili, alitambua kuwa kwa wasailiwa ambao walikiri kutumia nyimbo kujifunza Kiswahili, walisema kwamba nyimbo za dini, burudani na siasa ziliwasaidia kujifunza misamiati ya Kiswahili. Chimerah (1998) anasema kwamba fasihi inaashiria utamaduni wa mtu na huwa na

12.

muathiriano chanya ama hasi kwa yule anayepokea ujumbe wa msanii. Anaendelea kusema kwamba Muziki ulichangia sana maenezi ya Kiswahili Afrika Mashariki. Mmoja wa wasanii ambao walianzisha muziki Uganda wakitumia Kiswahili na Kiganda ilikuwa ni Sammy Kasule. Hata hivyo baadayae wana muziki tajika kama Joseph Mayanja (Jose Chameleon); Juliana Kanyomozi na wengine wametumia Kiswahili katika nyimbo zao. Aidha nyimbo humpa mjifunzaji lugha ya piili motisha na ari ya kufuatilia kile kinachoimbwa katika hali hii mtu anajifunza misamiati ambayo itamsaidia katika mawasiliano. Uganda ilichukua muda kuhalalisha ufundishaji wa Kiswahili darasani kwa sababu ya historia mbaya. Hivyo kwa wale walikutana na Kiswahili katika mazingira ambayo si rasmi mara nyingi walijitahidi kujifunza Kiswahili kupitia muziki wa wasanii mbali mbali.

Maoni yake Chimerah (2011), yalikuwa muhimu sana katika utafiti huu kwani yanaeleza bayana kuhusu mchango wa mziki katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili. Pengo lililopo ni kuwa uchunguzi wake haukujadili chochote kuhusu vijana wa leo, lakini tangu uchunguzi wake ulinukuu nyimbo pamoja na ujifunzaji wa Kiswahili, utafiti huu utaendelea kurejea jambo hili katika kufanikisha lengo la kwanza katika utafiti huu litakalohusu kutambua mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa loeo.

2.3 Yaliyoandikwa kuhusu uhusiano na tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa mwanakupona na ile ya vijana wa leo.

Erikson (1961), katika uchunguzi alioufanya kuhusu majukumu ya vijana katika jamii, alieleza kuwa majukumu ya vijana katika jam ii yamekuwa yakibadilika jinsi hali ya jam ii inavyoendelea kubadilika vilevile. Kwa mfano, katika mfumo wa maisha ya kiasili ya Mwafrika kabla ya maajilio ya wageni na elimu ya Kimagharibi, malezi ya vijana pamoja na kuwaelekeza katika jamii yalikuwa ni wajibu wajamii nzima. Hii ni kwa sababu watoto walikuwa ni mali yajamii.

Tabia potofu miongoni mwa vijana zilishutumiwa na watu wote kwa vile maisha yalikuwa ni ubia au ushirika. Watoto walikuwa chini ya jicho pekuzi la jam ii nzima kila wakati. Majukumu ya vijana vivyo hivyo yalikuwa bayana huku vijana wa kiume wakiandamana na wazazi wao wa kiume waliowafunza shughuli za kiume kama vile uwindaji na jinsi ya kuihami jamii hata kuikidhia familia yake mahitaji akishaoa. Wasichana nao walifundishwa mambo ya unyago yaliyozingatia utekelezaji kamilifu wa majukumu yao wakishaolewa. Katika hali hii ya maisha

ya kitamaduni, vijana hawakuwa na changamoto nyingi kwa sababu kulikuwa na utaratibu wa kuwaelekeza kulingana na kilajamii.

Maoni haya kama yanavyojadiliwa na Erikson (1961), yalikuwa muhimu sana katika utafiti huu kwa kuwa yamedhihirisha tofauti iliyopo kati ya hali ya Kiafrika pamoja na Kimagharibi pamoja na jinsi hali ya jam ii inavyoendelea kubadilika, hata hivyo, maoni yake yanaeleza kuwa na hata wasichana nao walifundishwa mambo ya unyago yaliyozingatia utekelezaji kamilifu wa majukumu yao wakishaolewa, anaendelea kueleza kuwa katika hali hii ya maisha ya kitamaduni, vijana hawakuwa na changamoto nyingi kwa sababu kulikuwa na utaratibu wa kuwaelekeza kulingana na kilajamii.

Pengo lililopo ni kuwa maoni yake Erikson (196 l), hayakujadili zaidi kuhusu suala la lugha, lakini uchunguzi huu utaziba pengo hili kwa kujikita kwa yaliyozungumziwa na Erikson iii kubainisha uhusiano na tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa mwanakupona na ile ya vijana wa leo.

Shah (2014) anasema mtu hawezi kupata maarifa mapya kutumia teknolojia na kujikita tu kwenye mawasiliano. Pia kujifunza lugha ya pili sio tu kujifunza sarufi na msamiati, ila ni kujifunza sauti mpya, kujieleza najinsi ya kutatua mambo, anaendelea kusema kwamba biashara nyingi hufanya pamoja na makampuni mengi kutoka nchi nyingi. Kwa hivyo, huajiri watu tofauti ambao wanaweza kuwasiliana kwa lugha tofauti na kuelewa tamaduni nyingi. Unaposomea kozi yeyote ile na ujifunze lugha ya pili utakuwa na umuhimu zaidi kuliko yule ana lugha ya kwanza peke yake. Ameendelea kutoa mfano kwamba ukiwa na makanika anayejua Kirusi na Kijerumani na mkuu wa kampuni ajuae Kijapani ama Kihispania, mhasibu ajuae Kifaransa na Kichina, atafanya kazi vizuri na watu wengi kuliko yule ambaye anajua lugha moja tu.

Maoni yake Shah (2014) yalikuwa muhimu katika utafiti huu, kwani yanaeleza kuwa mtu hawezi kupata maarifa mapya kutumia teknolojia na kujikita tu kwenye mawasiliano. Pia kujifunza lugha ya pili sio tu kujifunza sarufi na msamiati, ila ni kujifunza sauti mpya, kujieleza najinsi ya kutatua mambo, anaendelea kusema kwamba biashara nyingi hufanya pamoja na makampuni mengi kutoka nchi nyingi. Tofauti iliyopo ni kuwa alitumia mfano wa kibiashara anaposema kuwa ukiwa na makanika anayejua Kirusi na Kijerumani na mkuu wa kampuni ajuae Kijapani ama Kihispania, mhasibu ajuae Kifaransa na Kichina, atafanya kazi vizuri na watu wengi kuliko yule ambaye anajua lugha moja tu. Lakini tangu mfano huo utafiti huu ulijikita kwa matumizi ya

13.

lugha, utafiti huu utaendelea kurejea suala hili katika kukamilisha lengo la pili katika utafiti huu litakalohusu kubainisha uhusiano na tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa mwanakupona na ile ya vijana wa leo.

2.4 Yaliyoandikwa kuhusu kuchunguza jinsi uhusiano na tofauti za lugha kati ya lugha ya utenzi wa mwanakupona zinavyoweza kuchangia kukuza na kuendeleza Kiswahili miongoni wa vijana wa leo.

Kithaka wa Mberia (2004) akinukuliwa katika diwani ya Tunu ya Ushairi, anaeleza kuwa mfumo huu wa kiasili ambao ulijikita katika taratibu za tamaduni maalum ulivurugwa na majilio ya wakoloni pamoja na wageni wengine kutoka nchi za Kimagharibi. Mtagusano na wageni hawa ulivuruga utaratibu wa mifumo ya ulezi ambayo ilikuwako. Elimu ya Kimagharibi ilileta mambo mapya na hata kuvuruga thamani pamoja na maadili katika jamii. Kwa mfano vijana walilazimika kwenda shuleni na vilevile wazazi wao kutafuta kazi katika sehemu za miji iii kukidhi mahitaji mapya yaliyotokana na njia hizi mpya za maisha. Jinsi jam ii zetu zilivyoegemea zaidi kuelekea utaratibu wa maisha ya Kimagharibi ndivyo asasi zilizohusika moja kwa moja na malezi ya vijana katika jamii zilivyoendelea kuporomoka na hivyo kuwaacha vijana bila mwelekeo maalum wa kuwafunza maadili.

Maoni ya Kithaka wa Mberia (2004), yalikuwa muhimu katika utafiti huu wetu, kwani yanaeleza kuhu diwani ya ushairi, pia maoni yake yanaeleza kuhusu vijana. Pengo lililopo ni kuwa uchunguzi wake ulirejea diwani ya Tunu ya Ushairi, lakini tangu maoni haya yamekuwa na uhusiano baina ya lugha, ushairi pamoja na vijana, maoni yake Mberia yataendelea

kurejelewa katika utafiti huu utakaolenga kuchunguza mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini Uganda

Mutenyo.A. ldah, Deborah Nanyama Amukowa, Oka!, Benard Odoyo (2021) katika uchunguzi wao uliofanywa kuhusu Mitindo Ya Ujifunzaji Lugha Ya Pili Katika Kufanikisha ujifunzaji wa Kiswahili Kama Lugha Ya Biashara Mjini Kampala, Uganda, walieleza kuwa Shughuli za biashara nchini Uganda zilianza zamani za kale wakati wa ujio wa wakoloni na usambazaji wa Kiswahili. Kiswahili kilisambaa Uganda kupitia njia mbalimbali moja wapo ikiwa ni biashara. Kimsingi, maingiliano ya jamii zenye tamaduni na lugha mbalimbali hutokana na ushirikiano katika biashara na shughuli nyinginezo za kijamii. Shughuli hizo huzua haja za kuwepo kwa

lugha moja itakayoweza kuwaunganisha watu wenye tamaduni na lugha mbalimbali. Hivyo basi, uendelezaji wa biashara unakuwa mgumu bila matumizi ya lugha inayoeleweka na wengi. Kutokana na hali hii, kujifunza Kiswahili ama lugha ya biashara hakuepukiki.

Ingawa uchunguzi wa wataalamu hawa ulihusu biashara, lakini pia uchunguzi wao ulijadili kuhusu ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, na hata hivyo, maoni yao yalirejea suala la utamaduni, kwa hivyo yataendelea kutumiwa katika utafiti huu utakaohusu mchango wa utenzi wa mwanakupona katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini Uganda.

SURA YA TATU
MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii, utafiti huu, ulibainisha muundo wa utafiti, eneo la utafiti, mbinu alizotumia katika ukusanyaji wa data, utaratibu atakaoufuata katika wakati wa kukusanya data, uhakikishaji wa ubora, asili ya data, pamoja na uchanganuzi wa data.

3.2 Muundo wa utafiti.

Utafiti huu ulikuwa ni wa kimaelezo, yaani, data ziliundwa pamoja na kuchambuliwa kwa kutumia maneno au lugha ya kawaida ambayo inaweza kueleweka kwa urahisi.

3.3 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa wilayani Kabale nchini Uganda.Eneo hili limechaguliwa, kwa kuwa lina maktaba mbali mbali zilizoweza kuwa na asili ya data mwafaka. Utafiti huu ulichangua eneo hili kwa kuwa lina vijana wengi wanaoweza kutoa data mwafaka.

3.4 Mbinu za ukusanyaaji wa data

Utafiti huu ulitumia mbinu ya ushuhudiaji pamoja na matumizi ya maktaba kama inavyodhihirishwa hapa chini:

3.4.1 Ushuhudiaji

Hii ni mbinu ya kutazama jinsi vitendo fulani vinapofanyika halafu mtafiti anakusanya data zinazokusud iwa.

Mbinu hii ilichaguliwa na utafiti huu kwa kuwa ilisaidia kukusanya data nyingi zenye uhusiano na vijana wa leo.

3.4.2 Matumizi ya maktaba

Utafiti huu ulitumia maktaba mbali mbali katika harakati za kukusanya data zilizokamilisha utafiti huu. Utafiti huu ulitumia maktaba mbili za Chuo kikuu cha Kabale, maktaba ya umma katika Munisipali ya Kabale katika Tarafa la Mwanjari.

Mbali na maktaba hizo mbili za Kabale, utafiti huu ulijikita kwa maktaba tembezi iii kukusanya data zilizo nyingi katika michakato ya kukusanya data za utafiti huu.

3.5 Sampuli na Usampulishaji

Utafiti huu ulitumia maktaba tatu pamoja na mitandao ya kijamii katika ukusanyaji wa data.

3.5.1 Jumuiya ya uteuzi wa sampuli

Utafiti huu ulitumia uteuzi lengwa.kwa mujibu wa Enon (1998), anaeleza kuwa uteuzi lengwa ni ule wa mtafiti wa kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data anazohitaji. Mtafiti alitalii

tenzi za Kiswahili, na kuchagua utenzi wa rnwanakupona Aliona Utenzi huu na kufanya utafiti kuhusu utenzi huu.

3.6 Vifaa vya kukusanya data

Mtafiti alifanya utafiti na kueleza kuwa vifaa vya kukusanya data ni; kalamu na karatasi kwa ajili ya kuandika data za utafiti Tepu rekoda kwa ajili ya kupima, na vikorokoro kwa ajili ya kuhesabu, kamera na vifaa vyake vya kupiga picha.

3.7Utaratibu wa kukusanya data

Mtafiti alifanya ujitarnbulishaji wake kwa viongonzi wa maktaba tofauti akionyesha kibali chake cha utafiti halafu akatolewa na ruhusa uliornkubali kutumia maktaba hizo katika ukusanyaji wa data

3.8 Kuhakikisha ubora

Katika shughuli za ukusanyaji na utekelezaji, Data zilirejelewa zikahakikishwa kuwa zinaambatana na mada iii kukidhi rnalengo ya utafiti.

SURA YANNE
UCHANBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA 4.1

Utangulizi

Utafiti huu katika sura ya nne, ulikusanya data kutoka Maktaba, data hizo zilichambuliwa harafu baadaye, ziliwasilishwa kama ifuatavyo;

Hivyo pia, data zilizokusanywa, zilirejelea sana malengo matatu yaliyoongoza utafiti huu, malengo hayo yalikuwa ni pamoja na kutambua mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana, lengo la pili lilikuwa ni la Kubainisha uhusiano na tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa mwanakuponana na ile ya vijana wa leo. harafu lengo la tatu katika utafiti huu lilikuwa ni la kuchunguza jinsi uhusiano na tofauti za lugha katika utenzi wa mwanakupona zinavyoweza kuchangingia kukuza na kuendeleza Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo nchini uganda.

4.2.Data kuhusu kutambua mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo

Katika kutambua mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo utafiti huu ulijikita kwa mtindo wa jinsi utenzi huu ulivyotunzwa, harafu baadaye kutoa maoni ya kimahusiano. Mchango wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakupona katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo, nchini uganda, uchanganyaji wa lugha, mkopo wa lugha za kigeni, matumizi ya mitindo ya lugha kama vile tashibihi pamoja na matumizi ya wahusika katika matumizi ya lugha kama ilivyochanganuliwa hapa chini.

4.2.lKutumia misingi ya Kiswahili

Katika njia ya maktaba, utafiti huu ulibainisha kuwa lugha iliyotumiwa katika utunzi wa utenzi wa Mwanakupona ilijikita kwa misingi ya lugha yaani; kuhakikisha kwamba lugha imetumiwa kwa kuzingatia kanuni mwafaka zinazoeleweka na wasomi wa kazi, hapo katika kuchunguza jinsi lugha inavyoweza kukuza na kuendeleza lugha ya kiswahili miongoni mwa vijana wa leo, hivyo pia uchunguzi huu ulielewa kuwa ingawa vijana hawa hutumia lugha ya Kiswahili ikiwa na makosa, lakini huwa wanalenga kutoa ujumbe mwafaka kwa wenzio au hata wakilenga kuwasiliana na vijana wenzao au hata na mwanajamii yeyote katika jam ii. Na hivyo, utafiti huu kudhihirisha uhusiano wa namna hiyo wazi.

14.

4.2.2Uchanganyaji wa lugha

Hivyo pia katika uchambuzi wa data zilizopatikana katika utafiti huu, uchunguzi huu ulibaini kuwa kuna uhusiano wa uchanganyaji wa lugha, kwani uchunguzi huu uliendelea kutafakari mifano inayohusiana na suala hili, na hapo ilibaini kuwa katika utunzi wa utenzi wa Mwanakupona, mtunzi alitumia lugha ya Kiswahili akiichanganya na lugha nyingine kama vile lugha ya Kiarabu pamoja na lahaja za Kiswahili. Kwa upande mwingine, imedhihirika vile kuwa na hata vijana wa leo, huchanganya lugha ya Kiswahili pamoja na lugha nyinginezo za kikawaida ili kukamilisha mawasiliano yao na wanajamii wenzao.

4.2.3Mkopo wa Iugha za kigeni

Katika utenzi wa Mwanakupona, lugha za nje ya Kiswahili, zilitumika sana ambapo lugha kama vile Kiarabu, Kipemba na hata Kiunguja zilikopwa sana iii kuendeleza ujumbe uliolengwa kuwasilishwa na mtunzi wa utenzi huu. Hivyo utafiti huu ulivyofanya maakisio na lugha inayotumiwa na vijana wa leo, uchunguzi huu ulitambua kuwa na hata vijana wa leo hukopa lugha kama vile; Kiingereza, Kifaransa na hata Kiarabu vile katika mazungumzo yao ya moja kwa moja katika uendelezaji wa lugha ya Kiswahili.

4.2.4Matumizi ya mitindo ya lugha kama vile tashibihi

Katika uchunguzi huu pia, utafiti huu ulibaini uhusiano wa kutumia mtindo wa lugha. Utafiti huu ulitambua kuwa katika utenzi wa Mwanakupona ulitumia mbinu kama tashibihi pamoja na methali, hata hivyo, utafiti huu ulivyoendelea kutambua uhusiano, ulitambua kuwa na hata vijana wa leo hutumia sana mitindo ya lugha katika mawasiliano ya lugha ya Kiswahili. Mfano uliotambulika katika utenzi huu ni kama binti Mashamu alipomsihi mtotowe kupenda mmewe na kumutunza kama malaika.

4.2.SMatumizi ya wahusika katika matumizi ya lugha

Katika utafiti huu vile ulitambua kuwa katika utenzi wa Mwakupona ulijikita sana katika matumizi ya wahusika iii kuwasilisha ujumbe wa kusudi. Hapo pia uchunguzi huu katika kurejea suala hili, ulitambua kuwa na hata vijana wa leo hutumia wahusika katika mawasiliano yao ya kawaida. Hapo utafiti huu uliweza kudhihirisha uhusiano uliopo kati ya lugha katika utenzi wa Mwanakupona pamoja na lugha inayotumiwa na vijana wa leo.

4.2.6Matumizi ya lugha ya kuwakilisha mazingira

Katika lugha iliyotumiwa na mtunzi wa utenzi wa Mwanakupona, iliionyesha mazingira bainifu, yaani mazingira ya nyumbani na mazingira ya kupendana ambapo na hata katika uchunguzi huu,

na vijana walidhihirika kuwa wanatumia lugha ya Kiswahili katika mazingira mbali mbali kama vile shughuli za kifamilia, elimu na urafiki.

4.3.Data kuhusu kubainisha uhusiano na tofauti zilizopo kati ya Iugha ya utenzi wa mwanakupona na ile ya vijana wa leo

Katika data zilizohusu uhusiano na tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa Mwanakupona na ile ya vijana wa leo, utafiti huu ulidhihirisha uhusiano na tofauti zilizopo kati ya mtindo wa lugha, wahusika katika lugha, ugumu wa lugha, miaka ya lugha na mkopo wa lugha moja pamoja na tofauti ya uhariri kama ifuatavyo;

4.3.1 Tofauti zilizopo kati ya mtindo wa lugha

Uchunguzi huu katika uchanganuzi wa data, ulitambua kuwa utenzi wa Mwanakupona ulitumia mtindo wa lugha wa kiwango cha juu, yaani, mtindo wenye vifungu vigumu, aidha katika kuchanganua upande wa lugha inayotumiwa na vijana wa leo, uchunguzi huu ulitambua kuwa lugha ya vijana wa leo huwa ni lugha yenye mtindo rahisi yaani, mtindo unaoeleweka vizuri na mtumizi wa lugha yeyote ule. Hivyo, utafiti huu uliweza kutoa tofauti ya masuala haya mawili kwa kujikita kwa tofauti za mtindo wa lugha.

4.3.2Wahusika katika lugha

Katika uchunguzi huu uliofanywa kuhusu utenzi wa Mwanakupona, ilidhihirika kuwa utunzi huu ulitungwa kwa kutumia majina ya wahusika yenye uhusiano na lugha, kwa mfano, katika utenzi wa Mwanakupona, jina mwanakupona lenyewe lilibainika kuwa na maana ya mtoto wa kupona ambapo uchunguzi huu ulivyochunguzwa kiundani, uchunguzi huu ulitambua kuwa wao vijana wa leo hutumia wahusika bila kuzingatia msingi wowote wa kumpa mhusika jina, na hivyo, utafiti huu ulidhihirisha tofauti ya wahusika katika lugha inayotumiwa kati ya utenzi wa Mwanakupona pamoja na lugha inayotumiwa na vijana wa leo.

4.3.3Ugumu wa lugha

Kwa vile uchunguzi huu katika uchanganuzi wake katika uchunguzi huu, ulitambua kuwa lugha iliyotumiwa katika utenzi wa mwanakupona, ilikuwa na ugumu sana ikilinganishwa na lugha inayotumiwa na vijana wa leo. Kadhalika, lugha iliyotumiwa katika utenzi wa Mwanakupona ilipangwa kwa maana fiche hasa pale mtunzi alipotumia mashairi katika utunzi wa kazi zake, jambo hili ni tofauti najinsi mambo yalivyo katika lugha inayotumiwa na vijana wa leo.

15.

4.3.4Miaka ya lugha

Katika uchunguzi huu pia, changanuzi wa data ulidhihirisha kuwa lugha iliyotumiwa katika utenzi wa Mwanakupona ilizeeka sana, yaani ni lugha inayorejelewa kama lugha ya kizamani ambapo lugha inayotumika na vijana wa leo hurejelewa kama lugha ya kisasa. Tofauti ya miaka ya lugha inadhihirika pale ambapo utenzi huu ni wa miaka ambapo ulirejelewa kama kazi iliyomaliza wakati mrefu bila kuhariri wa ambapo vijana wa leo wanaaminika kuwa wanatumia lugha ambayo wanaipokea pamoja na kujifunza kutokana na njia za hivi sasa. Na kwa hivyo, utafiti huu ulidhihirisha tofauti hiyo ya miaka ya lugha.

4.3.51dadi ya lugha za mkopo

Idadi ya lugha za mkopo ilirejelewa katika utafiti huu katika kutambua tofauti iliyopo kati ya lugha iliyotumiwa katika utenzi wa Mwanakupona pamoja na lugha inayotumiwa na vijana wa leo, hivyo katika uchunguzi wa ziada kuhusu suala hili, uchunguzi huu ulielewa kuwa katika utenzi wa Mwanakupona, utunzi ulikopa msamiati kutoka kwa lugha ya Kiswahili ilihali lugha ya vijana wa leo hukopa msamiati kutoka kwa Kiingereza, Kiarabu pamoja na Kifaransa. Hivyo, utafiti huu ulidhihirisha idadi ya lugha za mkopo ikiwa mojawapo wa tofauti kati ya utenzi wa Mwankupona pamoja na vijana wa leo.

4.4. Ulinganuzi wa jinsi uhusiano na tofauti za lugha katika utenzi wa mwanakupon zinavyoweza kuchangia kukuza na kuendeleza Kiswahili miongoni mwa vijana wa I Utafiti huu pia uliendelea kuchunguza kuhusu jinsi uhusiano na tofauti za lugha katika utenzi wa

mwanakupona zinavyoweza kuchangia kukuza na kuendeleza Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo. Hivyo, uchunguzi huu ulidhihirisha kuwa ulinganuzi huo unateuliwa katika njia kama vile; kulenga kuangazia juu ya lugha ya Kiswahili, vyote hulenga kushughulikia mtindo wa lugha, kuhariri kwa lugha, miaka ya lugha ya Kiswahili pamoja na ukopaji wa lugha ya kutumiwa kama ilivyochunguziwa hapa chini:

4.4.2Kulenga kuangazia juu, ya lugha ya Kiswahili

Uchunguzi huu baada ya kuchunguza jinsi uhusiano na tofauti · za lugha katika utenzi wa mwanakupona zinavyoweza kuchangia kukuza na kuendeleza Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo, ulionyesha kuwa vyote hulenga kuangazia juu ya matumizi ya lugha, yaani lugha ya Kiswahili.

16.

4.4.2Vyote hulenga kushughulikia mtindo wa lugha

Uchunguzi huu baada ya kulinganisha na kulinganua tofauti na uhusiano kati ya lugha iliyopo katika utenzi wa Mwanakupona pamoja na lugha inayotumiwa na vijana wa leo, ulinganuzi huu ulielewa kuwa lugha zote hulenga kushughulikia mtindo wa lugha.

4.4.3Kuhariri kwa lugha

Uchunguzi huu baada ya kulinganisha na kulinganua tofauti na uhusiano kati ya lugha iliyopo katika utenzi wa Mwanakupona pamoja na lugha inayotumiwa na vijana wa leo, ulinganuzi huu ulitambua kuwa utenzi wa Mwanakupona umetolewa uhariri pamoja na wahariri mbali mbali, arnbapo na hata uchunguzi huu pia ulitambua kuwa hata na lugha ya vijana wa leo huwa ilijikta kwa lugha ya kisasa.

4.4.4 Miaka ya lugha ya Kiswahili

Ingawa uchunguzi huu ulijadili kuhusu kwa jinsi lugha ya utenzi wa Mwanakupona ilivyotumiwa kwa muda mrefu, lakini vile uchunguzi huu pia ulibaini kwamba kwa kiwango fulani, kuna usawa wa lugha ambapo kuna usawa wa misamiati, yaani kuna maneno yaliyodhihirika kuwa yanatumiwa katika lugha ya Mwanakupona, lakini vile kuna maneno arnbayo na hata maneno hayo yanatumiwa na vijana wa leo.

4.4.5 Ukopaji wa lugha ya kutumiwa

Uchunguzi huu baada ya kulinganisha na kulinganua tofauti na uhusiano kati ya lugha iliyopo katika utenzi wa Mwanakupona pamoja na lugha inayotumiwa na vijana wa leo, ulinganuzi huu ulitambua kuwa lugha zote hukopa lugha nyinginezo, kwa mfano katika uchunguzi huu, lugha ya utenzi wa Mwanakupona ilibainika kuwa inakopa lugha ya Kiarabu huku katika kurejea lugha inayotumiwa na vijana wa leo, uchunguzi huu ulibaini kuwa lugha ya vijana hukopa lugha ya Kiingereza, lugha ya kifaransa pamoja na lugha ya Kiarabu.

–~

SURA YATANO

MUHTASARI, HITIMISHO, NA MAPENDEKEZO

5:1 Utangulizi

Sura hii inasehemu Tatu ya kwanza inaelezea Muhtasari Hitimisho na Mapendekezo ya utafiti.

5:2 Muhtasari

Tasnifu hii imeundwa kw sura Tano yani sura ya kwanza,sura ya pili,sura ya tatu,sura ya nne a sura ya tano

Sura ya kwanza imeundwa kwa Usuli wa Mada,Suala la utafiti,Malengo ya utafiti,,lengo kuu,malengo mahususi,Maswali ya utafiti,umuhimu wa utafiti,Upeo wa utafiti,Upeo wa wakati,Upeo wa kijiografia na changamoto za utafiti.

Sura ya pili imeundwa kwa mapitiyo ya maandishi yani yalioandikwa kuhusu malengo yangu ya utafiti.

Sura ya tatu imeundwa kwa mbinu za utafiti, yani muhundu wa utafiti,Eneo la utafiti, Mbinu za ukusanyaji wa data ,Ushuhudiaji, Matumizi ya maktaba,Sampli na Usamplishaji,Jumuyiya ya uteuzi wa Sampul,vifaa vya kukuusanya data na kuhakikisha ubora

Sura ya nne imeundwa kwa uchambuzi wa uwasilishaji wa data yani data kuhusu malengo yangu ya utafiti yani, data kuhusu lengo ya kwanza ni kutumia msingi wa lugha ya Kiswahili, uchanganyaji wa lugha, mkopo wa lugha za kigenyi,matumizi ya lugha ya kuwasilisha mazingira na matumizi ya mitindo ya lugha.katika Data za lengo ya pili kuna tofauti zilizopo kati ya mtindo wa lugha,wahusika katika lugha,ugumu wa lugha,na miaka ya lugha. Katika Data ya lengo ya tatu ni kulenga kuangaziajuu ya lugha ya lugha ya Kiswahili, kuhariri kwa lugha,miaka ya lugha ya Kiswahili na ukopaji ya lugha ya kitumia.

Sura ya tano imeundwa kwa Muhtasari,Hitimisho na Mapendekezo yani kwa watunga mitaala, walimu na watafiti wa badaye.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulitowa hitimisho la kila lengo kwa mfano

Lego la kwanza lilihitimishwa kuwa na mchangu wa lugha iliyomo katika utenzi wa mwanakuponana katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo. yani uchanganyaji wa lugha,mkopo wa lugha za kigeni, kwa uendelezaji wa vijana wa leo.

Lengo la pili lilihitimishwa kuwa kuna uhusioanona tofauti zilizopo kati ya lugha ya utenzi wa mwanakupona na ile ya vijana wa leo. kwa kuwa kuna tofauti zilizopo kati ya mtindo yalugha,uhusianowa wahisika katika lugha na ugumu waq lugha.

Lengo ya tatu lilihitimishwa kuwa kuna jinsi uhusiano na tofauti za lugha katika utenzi wa mwanakupona zinavyoweza kuchangia kukuza na kuendeleza Kiswahili miongoni mwa vijana wa leo.kama kulenga na kuzingatia juu ya lugha ya Kiswahili,kuzingatia miaka ya lugha na kuhariri kwa lugha

5:4. Mapendekezo ya utafiti

Tunatoa mapendekezo kwa asasi na wadau mbalimbali.

5:4.1 Kwa watunga mitaala

Waanze kutenganisha dhana ya utenzi na dhana ya epiki kwani dhana hizo ni tofauti

5.4.2 Walimu

Walimu kwa ujmla yao wazingatie na waangalie kwa kiina tofauti zilipo kati ya utenzi na epiki iii wasiendelea kuzifundisha dhana hizo kimakosa.

5.4.3 Kwa watafiti wa baadaya

Utafiti huu kwa watafiti wa baadaye wanaweza kwenda maktaba na kutafiti kuhusu utenzi za Kiswahili kama utenzi wa mwanakupona,utenzi wa ALI-inkishafi na utenzi wa fumoliyongo.

MALEJELEO

Applebee,N.A. na wenzake (2000).The language of littrature. United States of America.McDo augal little.

Biebuyck D.P (1972) The epic as a Genre n Congo Orai Literature in DorsonE.N

Chalingha,E.N. (2013) "vigenzo vya Rut5hth Finnegan katika utennzi wa lianja. Dar esalam; Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ,32,82-91

Finnegan, J. C.(1970) . Oral Literature in Africa. Oxford;Clarendon

Enon, J.C. (1998). Education Research, Statistics andMeasusurement; Educational Psychology.

Mdungi,A.(2000). "Dhana ya Utenzi wa Mapokeo. "Zanzibar; Ministry of Education katika jarada la Elimu Zanzibar.Toleo na. 1 ;30-37.

Mulokozi, M.m (1996) fasihi ya Kiswahili.Dar eslam; Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (1999) Tenzi Tatu Za Kale. Dar eslam ;TUKI.

Senkoro,F.E.M.K.(1988) Utenzi Nadharia na Tahakiki. Dar eslam University.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988).Kiswahili Senkondari. Dar eslam;Taaasisi ya Ukuuzaji Mitaala.

TAKILUK ,(1981).Misingi ya Nadharia Kiswahili.Sweden; Berlings ,Arlovs Tanzania. Wamitila ,K.W (2002) Uhakiki wa Fasihi ;Misingi na vipengele vyake. Na Iirobi; Kenya Listhotho ltd.-(2008). Kazi ya Fasihi Nairobi; Vide Muwa Publisher.

Chimerah, R. (1998). Kiswahili; Past present and Future, Nairobi University Press.

Chimerah, R. (2010). Kiswahili: Past present and Future. Nairobi: Nairobi University Press Erikson, H. E.

(1961) Youth Change and Challenge.New York: America Academy of Art and Science.

Kaaru, M.G. (2008) Daftari la Ushairi. Kwa Mwanafunzi wa Shule ya Upili: Oxford University Press

Mberia, K wa (1997) Natala. Nairobi: Marimba Publications.(2001) Kifo kisimani. Nairobi: Marimba Publications. (1999) Maua kwenye jua la asubuhi. Nairobi: Marimba Pub I